Mwongozo Wa Mwanafunzi

9

# Utiifu Kwa Mwanadamu

## Kupalilia Moyo wa Unyenyekevu Kwa Viongozi



MVMM

Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya

# Utiifu Kwa Mwanadamu

## Kupalilia Moyo wa Unyenyekevu Kwa Viongozi

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwanafunzi

Toleo la Tano

MVMM
Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya

# Utiifu Kwa Mwanadamu

## Kupalilia Moyo wa Unyenyekevu Kwa Viongozi

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwanafunzi

Toleo la tano

Maandiko Yanayotumiwa Katika Kitabu Hiki Yametoka Kwa:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2023, Teen Challenge USA.

Masomo haya yanaweza kuchapwa na kupeanwa kwa ajili ya matumizi ya huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali pamoja, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwa mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo: *Obedience to Man, 5th edition*

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa ili kutumiwa makanisani, shuleni, katika huduma za gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vile vile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, kitabu cha kuongoza mafunzo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge
PO Box 511
Columbus, GA, 31902 USA
Barua Pepe:gtc@globaltc.org
Tovuti: www.globaltc.orgna
www.iTeenChallenge.org

MVMM
Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya

Tarehe ya Mwisho Kurekebishwa: 01-2023

# Yaliyomo

**Sura ya 1. Kweli za kimsingi za kuwatii viongozi wako ....4**

A. Umekuwa ukiishi maisha gani ya kuwatii viongozi wako? ....4

B. Ni kiongozi yupi wapaswa kumtii? ....6

C. Kukuza mtazamo wa kutii ....7

D. Msingi wa kumtii mwanadamu ni upendo ....11

E. Kanuni zitakazo kusadia kuwatii viongozi wako kwa upendo ....13

**Sura ya 2. Viwango vitatu vya utiifu ....15**

Kiwango cha 1. Tii kwa kuwa uliambiwa ufanye hivyo ....15

Kiwango cha 2. Tii na ugundue sababu kuu ambayo ilimfanya kiongozi wako akuambie ufanye ....17

Kiwango cha 3. Tii kwa hiari yako ....18

**Sura ya 3. Unapaswa kujibu vipi unapoongea na viongozi wako? ....20**

A. Usimlaumu au kumshtumu kiongozi wako ....20

B. Weka msingi wa jibu lako kwa maoni yako ....20

C. Sema kwa njia ambayo itamsaidia kiongozi wako kufikia malengo yake ....21

D. Weka malengo ya jinsi utakavyojibu ikiwa shida fulani itajitokeza ....21

E. Tenga muda maalum wa kuongea na kiongozi wako ....21

F. Mtegemee Mungu akupe nguvu ya kufanya jambo hili kwa usahihi ....22

**Sura ya 4. Unapaswa kufanya nini kiongozi wako akikwambia ufanye jambo ambalo sio sahihi? ....24**

A. Tathmini kwa makini kile umeambiwa kufanya ....24

B. Gundua sababu kuu iliyomfanya kiongozi wako kukuambia ufanye hivyo ....26

C. Ikiwa sababu kuu ya kile ambacho kiongozi wako amekuambia ufanye ni kwa wema wako (na si dhambi), una jukumu la kutii ....27

D. Ikiwa sababu kuu ya kiongozi wako kukuambia ufanye jambo hilo ni kukuingiza katika dhambi, basi una jukumu la kutomtii ....28

**Sura ya 5. Matokeo ya kutii na kutotii viongozi wako ....31**

A. Matokeo ya kuwatii viongozi wako ....31

B. Matokeo ya kutowatii viongozi wako ....34

# Sura ya 1
# Kweli za kimsingi za kuwatii viongozi wako

## A. Umekuwa ukiishi maisha gani ya kuwatii viongozi wako?

Kila mmoja wetu ana hadithi za kweli ya kuhusu viongozi wetu na jinsi walivyokuwa sehemu ya maisha yetu. Huenda una hadithi nzuri na za kutia moyo mno. Au kumbukumbu ya viongozi wako inaweza kuleta picha ya hali za uchungu zinazokuumiza sana.

Katika somo hili tungependa kujifunza kupitia yale umepitia maishani mwako siku zilizopita na kutizama kwa makini jinsi Yesu anavyotaka uhusiane na kuwajibu viongozi wako. Ukweli wa kimsingi ni kwamba Mungu anataka uwatii viongozi wako. Kwa hivyo uhusiano wako na viongozi wako umekuwa vipi?

### 1. Suala la kutotii

Sisi sote tumeshindana kwa kiwango fulani na kutotii. Kwa wengi wetu tatizo hili limeanza tukiwa wadogo. Wote tulikuja kwenye ulimwengu huu kwa hali ya kutotii. Hata kabla ya kujifunza kuongea, tulitambua mbinu ya kutotii. Na toka wakati huo tumekuwa tukinoa makali yetu ya kutotii.

Wengi walikuta miaka yao ya ujana ikiwa imejaa mivutano kati yao na wazazi na viongozi wengine. Maisha ya kutotii kila mara husababisha matokeo yaliyojaa machungu, na kadri tunavozidi kuzeeka, ndivyo matokeo yanavyozid kutuathiri vibaya.Watu wengi wazima wanaishi katika jela leo kwasababu ya kutotii kwao.

### 2. Mgogoro na viongozi

Ni migogoro mingapi ambayo umewahi kuwa nayo na viongozi wako inayohusu swala la kutotii? Na mara nyingi migogoro inayotokea kwa vijana pamoja na wazazi wao ni juu ya kutotii. Na kama migogoro hii haitatatuliwa, inaweza kufikia kiwango cha kuvunja mahusiano.

Tendo moja la kutotii laweza kukuongoza katika kitendo kingine cha kutotii. Ni rahisi kujiambia, “Najua kilicho bora kwangu na hakuna atakayebadilisha nia yangu”.

Unaweza kuwa na kumbukumbu ya machungu ambapo mmoja wa viongozi wako walikukosea. Kwa kuwa viongozi wengine hawawezi kuaminika haimaanishi upuuze kila kitu wanachosema. Bado una jukumu la kuwatii kwa njia ambayo Yesu angefanya kama angekuwa kwenye nafasi yako.

Kama Mungu angewaondolea mbali viongozi wote wasio wakamilifu, basi usingekuwa na viongozi. Na utakapokuwa kiongozi basi hata wewe angekutupilia mbali pia!

Mungu hunyosha mkono wake wa rehema kwetu sote. Na mistari yote inayozungumzia juu ya utii kwenye Biblia tumepewa na Mungu. Anafahamu hakuna hata mmoja wa viongozi wako ni mkamilifu, lakini bado anatuambia tutii viongozi wetu.

## 3. Tabia ya kutotii

Kutotii kunaweza kuwa ni sehemu ya maisha yako ya kawaida kiasi cha hata kutofikiria. Unapoendelea na maisha ya kutotii inaweza kuwa katika hali ya kawaida ya jinsi unavyohusiana na viongozi wako. Tabia mbaya inaweza kukita mizizi katika maisha yetu.

Mara nyingi viongozi wetu wanatumia aina mbalimbali za adhabu ili wajaribu kutubadilisha, wakati mwingine adhabu hizi hutuletea mabadiliko. Na wakati mwingine hazileti mabadiliko yeyote.

Kwa hivyo tutaelekea wapi kutoka hapa? Mungu hakukuweka hapa duniani kutatua matatizo yote maishani mwa viongozi wako. Lakini Mungu anataka ujifunze jinsi ya kuwatii viongozi wako ambao si wakamilifu kwa njia ambayo itamtukuza.

Somo hili lina mafundisho mazito. Mengi ya mafundisho haya huenda yakaenda kinyume na dhana ulizo nazo kuhusu utiifu na uongozi. Biblia inazungumzia kuhusu mabadiliko yanayotakiwa kufanyika baaada ya sisi kumpa Yesu maisha Yetu.
Waefeso 4:17-32 inazungumzia kuhusu kuachana na njia za kale na kujivalia maisha mapya.

Somo hili huenda litakupa fursa nyingi ya kuachana na tabia na nia za kale na kuanza kukuza zile zinazomtukuza Yesu. Njia ya kuifanya kwa mpango wa Mungu ndiyo njia iliyo bora katika maisha yako yajayo.

## 4. Ni kwa jinsi gani Mungu anatoshea katika maisha yako?

Kujifunza jinsi ya kutii viongozi wako kutaathiri moja kwa moja uhusiano wako na Mungu. Kama humpendi Mungu na hutaki kumtii, basi itakuwia vigumu kuwatii viongozi wako.

Hata hivyo, kama umetoa moyo wako kwa Yesu na kumfanya Kiongozi wa maisha yako, basi uko katika njia ambayo itafanya kuwatii viongozi wako kuwa jambo rahisi mno. Mungu anaweza kukupa uwezo wa kubadilika, ili uweze kujifunza jinsi ya kutii viongozi wako katika njia ambayo itamheshimu Mungu.

# B. Ni kiongozi yupi wapaswa kumtii?

Katika Warumi 13:1-7 Mungu anasema wazi kwamba ameweka watu wenye mamlaka juu yako. Mungu anasema uwatii.Ukikosa kuwatii viongozi wako, basi utakuwa unaenda kinyume na Mungu pia. Una wajibu wa kibinafsi kutii wote wenye mamlaka walio juu yako.

## 1. Viongozi wa serikali

Wapaswa kutii viongozi katika serikali, kutoka kwa Rais wa nchi yako hadi kwenye kiwango cha chini cha viongozi wa serikali za mitaa. Hii itakuwa ni pamoja na kila serikali, jimbo, na viongozi wa serikali za mitaa. Unatakiwa kuwatii wanaume na wanawake wanaowafanyia kazi viongozi hawa, kama vile polisi. Unatakiwa pia kutii sheria zilizotolewa na viongozi hawa wa serikali.

**Warumi 13:1-2**

**Kila mtu na atii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu, na ile iliyopo imeamriwa na Mungu.**

**2 Kwa hivyo amwasiye mwenye mamlaka hushindana na agizo la Mungu; nao washindanao watajipatia hukumu.**

**1 Petro 2:13-14**

**13 Tiini kila kiamriwacho na watu, kwa ajili ya Bwana; ikiwa ni mfalme, kama mwenye cheo kikubwa;**

**14 Ikiwa ni wakubwa, kama wanaotumwa naye ili kuwalipiza kisasi watenda mabaya na kuwasifu watenda mema.**

Kama uwewekwa katika kituo cha Teen Challenge na mahakama, una wajibu wa kutii hakimu na muda wa majaribio yako au afisa wa kifungo chako.

## 2. Wazazi

Biblia inasema waziwazi kwamba watoto wapaswa kuwatii wazazi wao. Angalia Waefeso 6:1-3 na Kutoka 20:12. Biblia haibagui kama wazazi wako ni Wakristo au siyo. Wewe wapaswa kuwatii hata kama wao siyo Wakristo. Mungu ndiye aliyekupa hao wazazi, hivyo waheshimu, wastahi, wapende na kuwatii.

**Waefeso 6:1-3**

**Watoto, watiini wazazi wenu kwa sababu wewe ni mali ya Bwana, kwa kuwa hili ni jambo la haki ya kufanya. 2 “Waheshimu Baba na mama yako.” Hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi 3 Kama utamheshimu baba na mama yako, ‘mambo yataenda vizuri kwa ajili yenu, na utakuwa na maisha ya muda mrefu duniani.’**

### 3. Mwajiri

Kama una kazi, una wajibu wa kutii mwajiri wako-mtu unayemfanyia kazi. Maadamu unamfanyia kazi una jukumu la kumtii.

Katika Sura ya Nne tutajadili kwa kina ni nini unapaswa kufanya ikiwa kiongozi wako atakuambia ufanye jambo ambalo unaona siyo sahihi. Hata hivyo, mara nyingi viongozi wetu hutuambia tufanye mambo yaliyo sahihi.

### 4. Kiongozi wa kiroho—mchungaji

Kama Mkristo mpya, ni muhimu sana ujihusishe na kuwa mshirika wa kanisa la mahali pamoja. Wapaswa kuwatii viongozi wako wa kiroho, kama vile mchungaji au mchungaji msaidizi. Ikiwa unafunza darasa kanisani unakoshiriki, basi pia unawajibu wa kutii kiongozi wa Idara ya Elimu ya Kikristo kanisani mwenu.

### 5. Viongozi wa eneo unaloishi

Ikiwa kwa sasa unaishi mbali na nyumbani, una wajibu wa kutii viongozi wa mahali unapoishi kwa wakati huu unakoita, ‘nyumbani.’ Kwa wengine hii inaweza kuwa na kituo cha Teen Challenge, bweni la chuo, au mahali sawa na hapo. Huenda ulipoingia hapa ulitia saini mkataba wa kutii viongozi na sheria za mahali hapa. Ilmradi upo hapa, una wajibu wa kutii wote wenye mamlaka juu yako. Hii inahusisha msimamizi mkuu, mwangalizi wa wanafunzi, walimu  na mfanyikazi yeyote aliye juu yako.

Moja ya siri ya kujifunza kutii viongozi wako ni kumtegemea Mungu kumtumia kila kiongozi anayekuja maishani mwako. Unaweza kuchagua kumwamini Mungu kwamba atatumia viongozi wako kufanya mambo yote mema aliyoyapanga maisha mwako. Kumtumaini Mungu ndio ufunguo. Mungu anaweza kufanya kazi kupitia viongozi wako wote, hata wale ambao siyo wakamilifu.

Sasa kwa kuwa tumetambua ni viongozi wapi twapaswa kuwatii, hebu tuangalie jinsi twaweza kujifunza kuwatii viongozi wetu. Mapambano mengi makuu ya kuwatii viongozi wetu yamejificha katika nia zetu.

## C. Kukuza mtazamo wa kutii

Moja ya hatua muhimu katika kujifunza kutii viongozi wako ni kukuza mitazamo ya kutii. Mitazamo hii yaweza kuwa tofauti sana na tabia ya kutotii ambayo imekuwa sehemu ya maisha yako kwa miaka mingi.

Hapa kuna mitazamo au tabia kadhaa ambazo hukufanya usiwatii viongozi wako kwa urahisi. Unaweza kuchukua dakika moja na kufanya tathmini binafsi ya maisha yako.

Jipe alama kwa kutumia kiwango cha 1 hadi mpaka 10 kwa kila mtazamo, ambapo kupata alama “10” inamaanisha ndiyo tabia yako kuu maishani, na mahali palipo na “1” kamwe hiyo siyo sehemu ya mtazamo wako maishani.

____ Mtazamo wa kulaumu (mtazamo wa kukosoa)

____ Mtazamo wa kuasi

____ Mtazamo wa kutoshukuru

____ Mtazamo wa uvivu

____ Mtazamo wa mwenye hasira

____ Mtazamo wa ukaidi

Mitazamo yetu huathiri pakubwa tabia zetu. Kama una aina yoyote ya tabia hizi za kutotii, kwa kawaida hujitokeza unapokuwa na shida na mojawapo wa viongozi wako. Ikiwa utaruhusu tabia hizi za uasi kutawala mawazo yako, basi matendo ya kutotii yatakuwa sehemu ya maisha yako ya kila siku.

Wakati unapoamua kuwa Mkristo, moja ya sehemu muhimu ya maisha yako inayohitaji mabadiliko ni mtazamo wa nia yako. Yesu anataka ujifunze jinsi ya kumtii, na kutii viongozi wako. Kuwa na mitazamo ya utiifu ni ufunguo wa kubadilisha tabia yako.

Wafilipi 2:5 inatuambia, “Lazima uwe na mtazamo huo ambao Kristo Yesu alikuwa. Nao.” Kwa hivyo ni aina gani ya mitazamo ambayo Yesu alikuwa nayo kwa wale waliokuwa katika mamlaka wakati alipokuwa hapa duniani? Hebu tuangalie mitazamo minne ya utiifu ambayo tunahitaji kukuza maishani mwetu.

## 1. Mtazamo wa kuheshimu

### a. Mtazamo wakuheshimu ni nini?

Kuonyesha heshima ina maanisha kumheshimu kiongozi. Kuwa na moyo wa heshima kwa kiongozi wako inamaanisha kwamba utakuwa mpole na mkarimu kwa mtu huyu.

### b. Unakuza vipi mtazamo wa kuheshimu?

Moja ya njia iliyo na nguvu zaidi kwa kukuza mtazamo wa kuheshimu viongozi wako ni kuelewa kwamba Mungu anafanya kazi katika maisha yako kupitia viongozi wako.

Unahitaji kutambua kwamba Mungu anatumia viongozi wako kukutengeza ili uwe mwanamume au mwanamke ambaye alikuumba uwe. Wapaswa kumuangalia kiongozi wako kama “mikono ya Mungu,” inayokuongoza na kukuelekeza.

Wakati unapowaona viongozi wako kama wawakilishi wa Mungu, unaweza kumwamini Mungu kuwatumia viongozi hawa kukusaidia. Unaweza kuwaheshimu viongozi wako sio kwa sababu wanastahili heshima zako, lakini kwa sababu Mungu anastahili heshima yako.Wakati unapo waheshimi viongozi wako, hakika unamuonesha Mungu kwamba unamheshimu.

# 2. Mtazamo wa utiifu

## a. Mtazamo wa utiifu ni nini?

Kinyume cha tabia hii kwa wengi wetu ni rahisi kutambua. Ni mara ngapi umejiambia, ‘Hakuna mtu yeyote ataniambia cha kufanya!’ Ni rahisi kuwapinga watu walio na mamlaka juu yako, wanapokuwa watundu. Lakini tabia hii huru lazima idhibitiwe.

Kuwa na mtazamo mtiifu ina maanisha unaelewa kwamba hujiongozi. Unatambua kwamba hakika unamtii Mungu wakati unapowatii viongozi wako. Angalia Wakolosai 3:23. Wakati unatumia moyo wa unyenyekevu, huwa kwa hiari unatafuta kibali cha Mungu kwa kila jambo unalofanya. Kuwatii viongozi wako ni njia moja ya kufanya hivyo.

Unapokuwa na mtazamo wa unyenyekevu wewe husema, “**Nataka** kutii kiongozi wangu.” Unachagua kumkubali mtu huyu kuwa kiongozi wako, na wewe kwa hiari unakubali kuwaruhusu kuwa na jukumu la kuwa kiongozi wako. Unakubali kwamba sheria ni sehemu muhimu ya maisha yako, na unakubali kufuata sheria ambazo kiongozi wako anakupa.

Kama unataka kuona mfano mkubwa wa moyo wa unyenyekevu katika kanuni na sheria, soma Zaburi 119. Ndiyo sura ndefu zaidi katika Biblia, na moja ya mada ya sura hii ni mtazamo wa upendo na kuheshima sheria ambazo Mungu ametupa.

## b. Je, waweza kukuza mtazamo wa unyenyekevu kwa njia gani?

Unakuza moyo wa unyenyekevu kwa kujiambia, “Nachagua kunyenyekea na kuwatii viongzi wangu”. Umechagua kujiweka chini ya ulinzi wa viongozi wako.

Jiambie kwamba, “Namuamini Mungu kunilinda wakati ninaponyenyekea kwa viongozi wangu”. Ikiwa umeshikilia kwa nguvu mkono wa Yesu, unaweza kuwa na amani moyoni mwako kwamba atakusadia katika kila hali hizi.

Tafuta njia za kuonyesha nia yako ya kuwatii viongozi wako. Unachagua kupata utimilifu wa furaha katika kuwatii viongozi wako, ukijua kwamba hili ndilo Mungu anataka ufanye.

Mkakati mwingine ambao unaweza kukusaidia kukuza moyo wa unyenyekevu ni kujiuliza, “Kama ningekuwa kiongozi, ningejua kwa jinsi gani ikiwa mtu huyu ni mnyenyekevu kwangu kama kiongozi?”

Usijaribu kufanya kazi ya kiongozi wako. Usijaribu kuiba majukumu ya kiongozi huyo. Muache aongoze. Unahitaji kuzingatia kutii, si kukosoa kila uamuzi viongozi wako wanafanya.

Mpe Mungu matarajio yako yote. Weka orodha ya mambo yote ambayo unatarajia viongozi wako wakufanyie, kisha uombe na umpe Mungu matarajio haya yote. Unapoweka tumaini lako kwa Mungu, atakupa kile unachohitaji.

## 3. Mtazamo wa shukrani

### a. Mtazamo wa shukrani ni nini?

Unakuza tabia ya shukrani unapochagua kuwa na furaha na viogozi wale ulio nao huku ukimshukuru Mungu kwa ajili yao kila siku.

Wakati unapokuwa na moyo wa shukrani, huwa una furaha ya kweli na unathamini kile viongozi wako wanafanya. Unatambua kwamba Mungu anawatumia kukufanya uwe mwanamume au mwanamke ambaye angependa uwe.

### b. Ni kwa jinsi gani waweza kukuza mtazamo wa shukrani?

Waweza kukuza tabia ya shukrani kwa kuchagua kuwa na furaha na viongozi ulio nao, na kumshukuru Mungu kwa ajili yao kila siku.

**1 Wathesalonike 5:18**

**Shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.**

Onyesha shukrani ya kweli kwa viongozi wako kila siku. Washukuru wakati wanapokushauri na wanapokukosoa.

## 4. Mtazamo wa utulivu

### a. Mtazamo wa utulivu ni nini?

Hii ni rahisi mno—kujifunza kuwa mtulivu! Unahitaji kujifunza kuwa mtulivu kwa njia mbili, (1) kwa kiasi cha maneno unayoyasema, na (2) kwa sauti ya juu kiasi gani unapoyasema

Ni kujifunza pia kuwa mtulivu kutoka **ndani** pamoja na **nje.** Ni mara ngapi umesikia mtu akisema “ Nimefadhaika sana” Kufadhaika ni ishara ya kuonyesha kwamba hauna moyo wa utulivu. Wapaswa kujifunza kutuliza mawazo na hisia zako.

**1 Petro 3:4**

**Bali kuwe na utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika, yani roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu.**

Aya hii imeandikwa kwa wake kuhusu tabia yao kwa waume wao. Hata hivyo, kanuni hii ni nzuri kwa kila mtu. Twapaswa sote kukuza moyo wa upole na utulivu. Mungu anaona hali ya kuwa mtulivu kuwa jambo la thamani sana. Ikiwa Mungu anasema jambo hili ni la thamani kwake, basi vivyo hivyo tunahitaji kulithamini maishani mwetu.

### b. Unakuza vipi mtazamo wa utulivu?

Unakuza tabia ya utulivu kwa kujifunza kutii viongozi wako bila kuwasengenya. Kuwa tayari kutii kwa sababu kwa urahisi uliambiwa ufanye hivyo.

Weka imani yako katika Mungu. Atakuwa na uwezo wa kufanya kazi maishani mwako kupitia kwa viongozi wako wasio wakamilifu ili kutekeleza kile anachotaka ufanye. Muamini Mungu kufanya hivi katika nyakati zile unapojua viongzi wako wanafanya makosa na mambo yasiyo mema.

Usibishane na viongozi wako. Usidai maelezo ya ni kwa nini ufanye jambo fulani kabla haujatii.

### Kwa muhtasari

Unapochunguza maisha ya Yesu, utakuta kwamba alikuwa na moyo wa utiifu maishani mwake. Alionyesha tabia hizi katika mahusiano yake na viongozi wake na pia katika uhusiano wake na Mungu.

Tabia hizi zote nne za utiifu ni ngumu kukuza. Lakini Mungu anaahidi kwamba atatusadia ikiwa tutaomba msaada wake. Hatua moja ya kimsingi ambayo husaidia katika kukuza tabia hizi za utiifu ni kuzijenga kwa kuweka urafiki na huyo kiongozi.

Hata hivyo, msingi ulio bora wa kujenga tabia hizi za utiifu maishani mwako ni uhusiano wako na Mungu. Kumpenda Mungu ni sababu iliyo bora sana katika kukuza tabia hizi za utiifu kwa viongozi wako.

Tabia hizi zote za utiifu zinakuzwa akilini mwako wakati unapotoa uamuzi. Unaamua kufanya tabia hizi sehemu muhimu ya mawazo yako wakati unapohusiana na viongozi wako. Unapokuza tabia hizi za utiifu maishani mwako, utaona ni rahisi kuwatii viongozi wako.

# D. Msingi wa kumtii mwanadamu ni upendo

Kile kinachopenya kwa kina ndani ya moyo wako huathiri kwa kiasi kikubwa jinsi itakuwa rahisi au vigumu kwako kuwatii viongozi wako. Jiulize swali hili: nia yangu ni ipi kwa kuwatii viongozi wangu?

- *Hofu ya adhabu?*
- *Ili kuwa katika upande ulio sawa na kiongozi wako?*

  “Ikiwa nitamtii mama yangu leo, huenda basi nitachelewa nje na marafiki zangu leo usiku.”

- *Hukumu?*

  Huenda umefanya jambo mbaya, hivyo kwa wakati huu uko mwangalifu kutii ukitarajia hili litawasaidia viongozi wako kukusamehe ikiwa utapatikana.

- *Upendo?*

  Nia hii hufanya kazi vyema katika kukuweka katika njia ya utiifu.

Msingi wa kumtii Mungu ni upendo—huu ndio msingi ulio bora sana wa kuyajenga maisha yako. Hii ni kweli pia katika kuwatii viongozi wako. Unaweza kutii kutokana na hofu, au wajibu, au kwa kulazimishwa. Lakini motisha bora ya kuwatii viongozi wako ni upendo. Upendo ndio ufunguo wa kutii.

Ukijifunza kuwatii walio na mamlaka juu yako, basi utakuwa na uwezo wa wakuwatii. Hili laweza kuonekana kuwa jambo lisilowezekana kwako—kuwapenda viongozi wako. Lakini hakuna lisilowezekana kwa Mungu. Anaweza kukupa moyo wa upendo kwa viongozi wako.

Upendo ukiwa motisha wako itakuwa rahisi kupinga majaribu ya kutotii viongozi wako. Lakini kuwapenda viongozi wako huanza kwa kuchagua—je, ungependa kukuza uhusiano wa kibinafsi na viongozi wako? Je, ungependa kujifunza kuwapenda.

## 1. Mungu alikwambia uwapende wengine kama vile unavyojipenda mwenyewe

Yesu alisema kuwapenda watu wengine ndiyo amri ya pili kuu katika sheria za Mungu. Kumpenda Mungu ndilo jambo kuu la pekee lililo muhimu sana. Unapotii sheria hii, basi utakuwa unatii amri zingine zote utakazopewa na watu hawa. Angalia Mathayo 22:39 na Marko 12:31.

## 2. Yesu alikwambia uwapende wengine sawa na vile unavyojipenda wewe

Yohana 13:34 na Yohana 15:12 inaweka wazi jambo hili. Wapaswa kuwapenda walio katika mamlaka na upendo sawa ambao Mungu anakupenda nao. Unahitaji msaada wa Mungu kufanya hivyo.

**Yohana 13:34**

**“Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane ninyi kwa ninyi.”**

**Yohana 15:12**

**Amri yangu ndiyo hii, Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi.**

Yesu hatakuamrisha kufanya kitu kisichowezekana. Na ameahidi kutusaidia tunapokuwa dhaifu.

## 3. Ikiwa huwapendi viongozi wako, hutaweza kuwatii

Baadhi ya watu katika mamlaka ni rahisi kuwatii, lakini wengine ni vigumu kuwatii. Ikiwa utaendelea kuwatii viongozi wako na Mungu, ni lazima ujifunze kuwapenda walio na mamlaka juu yako. Uhusiano wa upendo hufanya utiifu kuwa jambo rahisi sana.

Ikiwa unawachukia walio na mamlaka juu yako, itakuwa ni vigumu sana kwako kuwatii. Ikiwa una imani na walio katika mamlaka utaweza kuwatii bila wasiwasi kwamba wanajua kilicho bora kwako. Ikiwa unawachukia viongozi wako, utakuwa na wakati mgumu

kuwaamini. Kanuni za kumtii Mungu zinaenda sawa na kuwatii viongozi wetu wanadamu. Angalia pia Yohana 15:10 na Yohana 14:21, 23-24.

# E. Kanuni zitakazo kusadia kuwatii viongozi wako kwa upendo

Je, kumekuwepo nyakati katika maisha yako ambapo ilikuwa vigumu kuwatii wazazi au watu walio na mamlaka juu yako? Je, kumekuwa na wakati ambapo ulisema, "Najua hawanielewi!" Pengine huwaelewi. Hebu tuangalie mambo machache ya kutusaidia kuelewa wale walio katika mamlaka.

## 1. Jifunze kumheshimu aliye katika mamlaka hata kama ana udhaifu

Sote hufanya makosa.Sote tuna makosa, mapungufu, shida za kihisia, na matatizo mengine mengi. Viongozi wako si wakamilifu. Lakini waheshimu licha ya udhaifu wao. Ikiwa unawaheshimu na kuwatii tu viongozi ambao hawana makosa, mwishowe hauta mheshimu mtu yeyote. Unachagua kuwaheshimu viongozi wako. Huwezi kumlaumu mtu yeyote kwa tabia yako ya kutowaheshimu viongozi wako. Katika 1 Petro 2:17, Mungu anatuagiza kuonyesha heshima kwa wengine.

**1 Petro 2:17**

**Waheshimuni watu wote. Wapendeni ndugu. Mcheni Mungu, Mpeni heshima mfalme.**

Ikiwa huwaheshimu viongozi wako, itakuwa vigumu kuwaelewa na kuwapenda. Utakuwa pia na wakati mgumu kuwatii.

## 2. Mungu hutumia viongozi kukuongoza na kukulinda


Warumi 13:1-2 inasema wazi kwamba Mungu ameruhusu viongozi ulio nao kuwa na mamlaka juu yako. Mungu amewaweka hawa viongozi juu yako ili wakupe mwongozo, wakusaidie, na kukulinda. Wao ni "mikono ya Mungu," ili wakufanye uwe chombo ambacho Mungu anataka uwe. Mungu amewapa viongozi wako majukumu mengi ambayo yanakuhusu moja kwa moja. Ilimradi utaendelea kuwatii viongozi wako na Mungu, utaendelea kuwa chini ya ulinzi wao. Mungu atatumia viongozi wako kukuelekeza maishani.

**Waebrania 13:17**

**Watiini wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea; maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili kuwa wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua; maana isingewafaa ninyi."**

Unapochagua kuwatii viongozi wako, Mungu anasema uko chini ya ulinzi wao—na ulinzi wake. Ni kama kusimama chini ya mwavuli wakati kunaponyesha. Wakati unapowatii

viongozi wako ni kama kusimama chini ya mwavuli wao. Ilimradi unatii, hutalowa maji, lakini ukichagua kufuta njia yako ya kutotii, basi utakosa ulinzi wao.




Mfano mwingine ambao umetumiwa kuelezea jinsi Mungu huwatumia viongozi ni matumizi ya nyundo na patasi katika kutengeza almasi. Mungu hutumia viongozi wetu kama nyundo na patasi ili kuondoa maeneo yasiyotii katika maisha yetu. Unaporuhusu utaratibu huu kuendelea, utafunua urembo wa kina ambao Mungu ameweka ndani yako. Utiifu ndiyo njia ya kuwa kile ambacho anataka uwe.

## 3. Itakuwaje kama hauwaamini viongozi wako?

Ni mara ngapi umesema, “Mimi siwaamini wazazi wangu” au “Simuamini kiongozi huyo”? Mara nyingi mtu anayejihisi hivi huwa amechukua jukumu ambalo hajapewa.

Kwa kawaida kiongozi huyu huwa amechukua jukumu la kumtathmini kiongozi ambaye yuko katika mamlaka—akimchunguza kiongozi kuona kama anafanya kazi yake. Ikiwa umefanya hivi hapo awali, basi bila shaka uligundua kwamba kiongozi wako hufanya makosa. Kwa kawaida itikio la utambuzi huu ni kusema kwamba, “Ikiwa viongozi wangu hufanya makosa (wana makosa, mapungufu n.k), basi lazima niwe muangalifu. Huenda akanipotosha! Siwezi kumuamini!”

Wakati unapokosa kuwaheshimu viongozi wako, itakuwa ni vigumu sana kwako kuwatii. Mungu hajakupa jukumu la kutathmini viongozi wako. Watu wengine wana jukumu hilo. Unapaswa kuzingatia kutumikiza majukumu yako kwa Mungu na viongozi wako—watii, waheshimu na kuwapenda viongozi wako.

# Sura ya 2
# Viwango vitatu vya utiifu

Katika kujifunza jinsi ya kutii viongozi wako, kuna viwango vitatu muhimu (hatua, au vipindi) vya kukua katika utiifu, ambavyo unahitaji kuvielewa na kuvitekeleza maishani mwao.

Tunaweza kulinganisha viwango vitatu vya utiifu kwa utii kwa shule. (Kiwango cha kwanza – shule ya msingi; kiwango cha pili – shule ya sekondari; kiwango cha tatu – chuo kikuu.) Ni lazima ukamilishe shule ya msingi kabla ya kuingia shule ya sekondari n.k.

Viwango vyote vitatu vya utiifu vinategemeana. Ni lazima utekeleze kiwango cha kwanza kabla ya kufikia kiwango cha pili. Ni lazima utekeleze hatua za kwanza na pili kabla ya kwenda hatua ya Tatu.

## Kiwango cha 1. Tii kwa kuwa uliambiwa ufanye hivyo

Hatua ya kwanza ya kutii ni rahisi kuelewa, lakini ngumu kuitekeleza maishani mwako. Kutii – kikomo – kwa kuwa uliambiwa uifanye japo inaenda kinyume na unavyokata kiasili. Hapa kuna baadhi ya mapendekezo ya jinsi ya kutekeleza hili maishani mwako.

a. Usilalamike Wafilipi 2:14-15

b. Usimjibu au kubishana na kiongozi wako. Waebrania 13:17

c. Fanya kazi uliopewa kwa njia *bora* kadri unavyoweza. Wakolosai 3:23

d. Jifunze kufurahia kutii.

Wakati unapofanya kazi katika kiwango hiki cha utiifu, basi uko katika njia inayokupeleka ukaribie kuwa mtu ambaye Mungu anataka uwe. Jambo kuu hapa ni kwamba umeamua kuwatii viongozi wako. Huenda katika siku zilizopita uliamua kutowatii viongozi wako bila hata kufikiria kuhusu jambo hili. Lakni kama utamfuata Yesu na kumfanya awe kiongozi wa maisha yako, basi inakupasa uitikie hali za kila siku za maisha kwa njia ambayo anataka uitikie. Kuwatii viongozi wako ni njia mojawapo ya kimsingi ya kuonyesha kwamba unataka kumfuata Yesu.

Wakati unapotii katika kiwango hiki, inakuwa ni fursa kwako kukuza tabia za kutii, na kuzitupilia mbali tabia za kutotii maishani mwako. Swala la kuwatii viongozi wako huanzia kichwani mwako—unafanya uamuzi. Wakati mwingine huonekana kama vita vinaendelea

ndani yako. Kila wakati unapoamua kuwatii viongozi wako, unapiga hatua moja ya kuwa mtu alieyekomaa ambaye Mungu anataka uwe.

Ikiwa tabia hizi za utiifu zitakua maishani mwako, unahitaji kujiambia, “Nataka kuwatii viongozi wangu.” Hii ndiyo inavyomaanisha kukuza shauku zinazompendeza Mungu. Lakini watu wengine wana vita vinavyeondelea akilini mwao. “Ikiwa nilisema nataka kuwatii viongozi wangu, nitakuwa nasema uongo, kwa kuwa sitaki kumtii kiongozi huyo.”

Kila wakati kiongozi wako anakuambia ufanye kitu fulani huwa ni fursa kwako kuchagua. Waweza kujiambia, “Nitamtii kiongozi wangu.” Hata kama hujihisi kutii, waweza kuamua kutii. Waweza kujiambia kitu cha kufanya.

Unapaswa kukua kiasi cha kwamba itikio lako la kawaida maishani litakuwa, “Nitatii” wakati kiongozi anapokuambia kufanya jambo.

## Utiifu mpofu

Lakini kutii katika kiwango cha kwanza sio utiifu mpofu. Katika kiwango hiki unatakiwa kuwa makini, na kufikiria kwa kina. Unahitaji kumtegemea Yesu akusaidie kutii, na kukusadia jinsi unaweza kukuza tabia za utiifu—mawazo ya utiifu utakayotumia wakati huu na siku za usoni.

Utiifu mpofu waweza kuwaelekeza watu kwa njia hatari. Kiongozi wa Doug alimuambia apeleke ujumbe kwa mtu mwingine. Lakini katika kujiandaa kutii, aligundua ana shida. Kwa hivyo akarudi kwa kiongozi wake na kumuuliza, “Je, unaniambia nimdanganye mtu huyu?” Mara moja kiongozi wake akabadilisha maagizo aliyompa Doug ili kusema uongo.

Utiifu mpofu kamwe hauachi kuuliza, “Jambo hili ni sawa kufanya?” Utiifu mpofu hupuuza kabisa kuzingatia matokeo ya kutii.

Mungu hatafuti utiifu mpofu. Anatafuta utiifu wenye uangalifu, utiifu ulio na akili. Wakati mwingine huenda tusielewe ni kwa nini viongozi wetu wametuomba kufanya kitu fulani. Twahitajika kuitikia hali hiyo kwa moyo ulio hiari kutii.

Katika sura ya 4 tutachunguza kwa kina kuhusu kile watakiwa kufanya wakati kiongozi wako anapokuambia ufanye jambo ambalo unaamini si sahihi.

Wakristo wengi hushindana na suala la kutii, sio kwa sababu wana viongozi waovu, lakini kwasababu wana historia ya kutotii. Hawataki mtu yeyote kuwaambia jambo la kufanya. Wanataka kujifanyia maamuzi yao wenyewe. Lakini ukweli ni kwamba—Mungu amewaweka viongozi maishani mwako ili wakusaidie. Kadri unavyozidi kuwasaida, ndivyo kwa haraka unavyozidi kuwa yule mtu Mungu angependa uwe.

Jambo kuu katika kiwango cha kwanza ni kuamua kutii. Ikiwa utachagua kuwatii viongozi wako, uko katika njia ya kushika kwa ustadi kiwango hiki cha utiifu.

Lakini kiwango cha kwanza sio mahali pa kukomea katika utiifu. Ni kiwango cha kuanzia tu, na sote tunahitaji kwendelea zaidi na kufikia kiwango cha pili.

# Kiwango cha 2. Tii na ugundue sababu kuu ambayo ilimfanya kiongozi wako akuambie ufanye

Kiwango cha Pili cha utiifu kinahusisha zaidi ya kutii. Pamoja na kutii kiongozi wako, unatumia akili yako. Kiwango cha pili kinahitaji kufikiria. Jifunze kutii na jaribu kufahamu jinsi kiongozi wako anavyofikiria. Gundua sababu kuu ya kwa nini kiongozi wako alikuambia utekeleze wajibu huo.

### a. Ni kwa jinsi gani nitatambua sababu kuu ya kwa nini kiongozi wangu ameniambia nifanye kitu fulani?

1) Jiweke katika nafasi ya kiongozi wako na utazame jambo hilo kwa mtazamo wao.

2) Muulize kiongozi wako ni kwa nini anataka ufanye jambo hilo.

   **Onyo:** Kuwa mwangalifu kuhusu ni **lini** utamuuliza kiongozi wako swali hili na uwe mwangalifu **jinsi** utakavyouliza.

   **Lini?** Kwa kawaida ni vyema kusubiri hadi wakati ujao ili ndipo umuulize kiongozi wako. Ikiwa utadai kiongozi wako akueleze sababu ya wewe kufanya hivyo *kabla* hujaanza kutii, basi kiongozi wako huenda akaona swali lako kuwa kama kupinga mamlaka yake.

   **Vipi?** Muulize kiongozi wako kwa njia inayoonyesha unataka kujifunza jinsi ya kutii vyema. Usiulize kwa njia inayoonyesha unapinga mamlaka ya kiongozi wako. Uliza, kwa nini jambo hili ni njema kulifanya? Usiulize, “Kwa nini nifanye hivi?”

3) Jaribu kugundua sababau kuu ambayo Mungu anataka ufanye jambo hili. Ni udhaifu upi (mapungufu) ambao Mungu anajaribu kukuonesha kupitia viongozi wako? Ni tabia ipi ambayo Mungu anajaribu kujenga maishani mwako kupitia kwa viongozi wako?

4) Waulize viongozi wako ni malengo yapi walio nayo kukuhusu.

Katika Bibilia kuna mifano mingi ya watu walioamua kuwatii viongozi wao. Danieli alikuwa kijana mdogo, huenda alikuwa chipukizi alipochukuliwa mateka katika nchi nyingine. Katika hali hii mpya alichaguliwa kujiunga na shule maalum ili kuandaliwa kufanya kazi serikalini. Katika siku ya kwanza kabisa alikumbana na shida kubwa mno. Chakula aliochopewa kula kilivunja sheria ambazo Mungu alikuwa amewapa watu wake.

Danieli alionyesha umakini mkubwa kwa kuitikia kwa njia iliyoonyesha wazi ni kwa nini alikaidi amri alizopewa. Alipata njia bunifu ya kuwajibu viongozi wake bila kutenda dhambi kwa Mungu. Soma hadithi hii katika Danieli sura ya 1.

### b. Kwa nini nigundue sababu kuu ya kiongozi wangu kuniambia kufanya jambo fulani?

Unapaswa kugundua sababu kuu ya kwa nini kiongozi wako amekuambia kufanya jambo fulani, ili uweze kwenda katika kiwango cha Tatu—na utii kibinafsi bila kuambiwa.

Sababu kuu ya wewe kufanya kazi katika Kiwango cha Pili ni ili upate kujifunza kukua. Mungu anakutaka uwe na ufahamu ulio bora kuhusu utiifu. Unafanya hii kwa kujifunza kuona hali hizi kwa mtazamo wa kiongozi wako.

Kiwango cha Pili cha utiifu hukupa fursa ya kukuza tabia za utiifu. Unaendelea kujiambia, "Nataka kuwatii viongozi wangu." Unapogundua sababu kuu ya kwa nini walikwambia ufanye jambo fulani, unajipa fursa ya kuwa na uelewa mwema wa njia bora ya kuitikia.

Sio kila kiongozi ana sababu kamilifu ya kukuambia ufanye jambo fulani. Wakati mwingine sababu kuu ambayo wanataka ufanye jambo ni tofauti na ile ambayo Yesu angesema ikiwa angekuwa katika nafasi ya kiongozi wako. Lakni wapaswa kuendelea kuwatii viongozi wako isipokuwa tu ikiwa sababu kuu ni wao kukuingiza katika dhambi. Tutazungumzia hili kwa mapana katika sura ya 4.

Ikiwa kiongozi wako hayuko tayari kujadili nawe sababu za kukupa jukumu fulani, basi kubali wajibu huo na endelea kutii. Usijigeuze kuwa hakimu ambaye anatoa hukumu kwa ajili ya sababu hizi kabla hujaamua kutii. Unaweza kumuomba Mungu akusaidie kuelewa sababu kuu hata kama kiongozi wako amekataa kukuelezea.

Zingatia kukua kwako kibinafsi. Kutii katika kiwango cha Pili ni hatua ya wewe kuwa yule mtu ambaye Mungu anataka uwe. Lakini usikome katika Kiwango cha Pili. Songa mbele hadi kiwango cha tatu cha utiifu.

## Kiwango cha 3. Tii kwa hiari yako

Kiwango cha Tatu cha utiifu ni wewe kutii kwa hiari yako kwa maana ni jambo sahihi kufanya.

Hili lapaswa kuwa lengo lako—Kujifunza kutii katika maeneo yote ya maisha yako. Unatii bila kuambiwa. Unatii kwasababu unataka kufanya jambo lililo sahihi. Unatii kwa sababu unajua kuwa hili ni jambo sahihi kufanya.

Watu wengine hutaka kuruka mara moja hadi kiwango cha Tatu—wakifanya marekebisho machache.Wanataka wajitegemee, wajiwekee masharti yao wenyewe, na kufanya tu kile wanataka kufanya. Lakini, hilo silo ambalo liko katika kiwango cha tatu. Wakati unapoishi katika Kiwango cha Tatu, bado upo chini ya mamlaka. Japo, utiifu wako huja mara nyingi kabla ya kiongozi wako kukuuliza ufanye jambo.

Mtu anayeishi katika Kiwango cha Tatu cha Utiifu huwa mwepesi wa kutii. Huwa hawatii kama uchaguzi wa mwisho. Hawasitisiti kutii. Wako makini na huuliza, "Naweza kutii kwa njia gani". Wako pamoja na viongozi wao, wakiwasikiza kwa makini.

Kuamua kutii kibinafsi ni hali ya kuonyesha kujidhibiti. Pia ni njia ya kuonyesha uhuru wa kweli. Dhana ya Mungu kuhusu uhuru siyo kufanya kile unachotaka kufanya, lakini kufanya kwa hiari kile anachotaka ufanye.

Mtu anayetii kwa hiari yake katika maeneo yote ya maisha yake ni mkamilifu. Yesu ndiye mtu wa pekee aliyefanya hivyo maishani mwake mwote. Tayari sote tumekosa, lakini twaweza kukusudia kufikia lengo hili. Kadri unavyozidi kutii kibinafsi, ndivyo unavyozidi kuwa kama Kristo. Utahitaji msaada wa Roho Mtakatifu ili uweze kutii kibinafsi. Yuko tayari kukusaidia na kukupa nguvu ya kutii kibinafsi.

Shida moja – kutii kivyako kwawezekana bila mabadiliko halisi kufanyika ndani. Unaweza kujikuta ukiishi katika kiwango cha chini kinyume na vile Mungu alikukusudia uishi. Unaweza kutii ili uepuke matokeo ya uchungu yanayotokana na kutotii. Mungu anatufata mambo zaidi. Anataka kukuona ukiwa umekua na kukuza tabia ya ndani ambayo ni alama kuu ya kweli ya mfuasi wa Yesu.

Utiifu unaweza kuleta mipaka mizuri maishani mwako huku ukikuza tabia ya kiungu. Hata hivyo, unatakiwa utambue kwamba Mungu anatafuta zaidi ya tabia ya utiifu—Mungu anakupenda na anataka kuwa na uhusiano wa kina na wewe.

# Sura ya 3
# Unapaswa kujibu vipi unapoongea na viongozi wako?

Katika mahusiano yako na viongozi wako, kutakuwa na wakati mwingi ambapo itabidi uwajibu. Njia iliyo sahihi ya kuwajibu viongozi wako kama Mkristo ni ipi? Unapaswa kusema nini? Unapaswa kusema kwa njia ipi?

Jinsi unavyowajibu viongozi wako ni eneo muhimu sana la wewe kuelewa. Migogoro mingi na viongozi imejikita katika suala hili. Ni mara ngapi jibu lako kwa viongozi wako limefanya mambo yakawa mabaya zaidi? Ni kama kumwaga mafuta kwenye moto. Ikiwa utajibu visivyo, waweza kufanya hali ikawa mbaya, wala sio bora.

Hapa kuna miongozo ambayo itakusaidia kupanga kile utakachosema kwa viongozi wako. Huenda ukawa na siku kadhaa au saa za kupanga kile utakachosema. Wakati mwingine utakuwa na sekunde au dakika chache tu za kujiandaa. Unapojifunza jinsi ya kuwajibu viongozi wako hii itakuasidia kuwa na uhusiano mwema nao, na itakuwa rahisi kuwatii.

## A. Usimlaumu au kumshtumu kiongozi wako

Hakikisha kwamba una tabia za kutii wakati unapojibu. Usiseme, “ulikosea katika.…”

Wapaswa kuwa mwangalifu kuongea na kiongozi wako kwa njia ya kuonyesha una moyo wa kufundishika—unataka kujifunza. Jukumu lako sio kumkosoa kiongozi wako.

Kwa kuamua jinsi utakavyomjibu kiongozi wako, waweza kuomba ruhusa ya kuuliza swali kuhusu lile jambo umeambiwa kufanya. Au waweza kuomba ruhusa ya kutoa maoni. Ikiwa viongozi wako watasema, “La” basi wapaswa kusonga mbele na kufanya kile ulichoambiwa kufanya.

Njia mojawapo ya kuomba kusikizwa ni kuuliza swali hili: “Naomba unisadie kuelewa vyema…?”

## B. Weka msingi wa jibu lako kwa maoni yako

Anza maoni yako kwa kusema, “Nafikiria hili…” au, “Kwa maoni yangu….” Usianze kwa kusema, “*Kila Mtu* anajua hii ndiyo njia sahihi ya kufanya…” au, “Akili ya kawaida inakuambia kwamba….”

## C. Sema kwa njia ambayo itamsaidia kiongozi wako kufikia malengo yake

"Ikiwa ungenielezea jambo hili tena, nadhani naweza kufanya kazi kwa njia sahihi."

Twapaswa kutoka katika ulimwengu wetu mdogo na kuangalia kile kinachoendelea katika mtazamo mkubwa. Kiongozi wako anajaribu kutimiza nini?

Kijana mmoja alikuwa akijadiliana na baba yake. Baba yake akamuuliza, Unafikiri sababu kuu ya mimi kukuambia 'la' ilikuwa gani? Alifikiri kwa muda mfupi kisha akasema, "Unajaribu tu kuyafanya maisha kuwa magumu."

Msichana huyu mdogo alikuwa amefungwa na matakwa yake mwenyewe kiasi ambacho alielewa kuwa sababu ya pekee ya mtu kutaka kumzuia ni kutaka kujaribu kufanya maisha yake kuwa magumu.

Unahitaji kuwapa heshima viongozi wako, na uelewe mara niyngi wana sababu nzuri ya kile wamekuambia ufanye.

Njia nyingine tekelezi ya kuelewa dhana hii ni kujiuliza, "Kama ningekuwa kiongozi katika hali hii, kwa nini ningeendelea kumuuliza mtu huyu kufanya jambo hili? Ningependa waitikie vipi katika uongozi wangu?" Maswali haya yaweza kukusaidia kupokea ukweli mpya wa jinsi ya kuwatii viongozi wako.

## D. Weka malengo ya jinsi utakavyojibu ikiwa shida fulani itajitokeza

Kuishi pamoja na aina fulani ya viongozi kunakupa fursa ya kujifunza mambo wanayo yaweka mbele na mambo yanayowakasirisha. Badala ya kufikiria, "Viongozi wangu wanahitaji kubadilika," tafuta njia za kuwajibu kwa moyo wa Kikristo. Unapoona vigumu kutii, mtazamo wako sharti ukazie jibu utakalotoa, sio kujaribu kumbadilisha kiongozi wako.

Chukua muda wa kufikiria jinsi utakavyojibu wakati utakumbana na hali ngumu kati yako na viongozi. Kwa mfano: "Ninapokasirika,

1. Nitanyamaza."
2. Nitajaribu kuchunguza ni kwa nini nilikasirika."
3. Nitajaribu kuliangalia suala hilo kupitia mtazamo wa kiongozi wangu."

## E. Tenga muda maalum wa kuongea na kiongozi wako

Kuna hali zingine ambazo unajua unahitaji kwenda kuongea na kiongozi wako. Ni rahisi kuhairisha na kusema, "Nitasubiri siku ambayo mambo yatakuwa sawa." Usisubiri wakati bora. Nyenyekea, na nenda usuluhishe mambo haraka iwezekanavyo.

Kwa mfano, "Baada tu ya kifungua kinywa nitakwenda kwa kiongozi wangu kumzungumzia kuhusu… Hili ndilo nitakalosema…."

# F. Mtegemee Mungu akupe nguvu ya kufanya jambo hili kwa usahihi

Kujifunza kuwajibu viongozi wako kwa njia sahihi—jinsi Mungu anavyotaka ujibu—yaweza kuonekana jambo lisilowezekana kwako. Kwanza, wapaswa utambue kwamba tabia za kutotii zimekita mizizi maishani mwako kwa muda mrefu, na wakati mwingine tabia hizi za kale huwa ngumu kubadilika.

Paulo anaeleza mashindano haya maishani mwake katika Warumi sura ya 7.

**Warumi 7:14-25**

**14 Kwa maana twajua ya kuwa Torati asili yake ni ya rohoni, bali mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi. 15 Maana sijui nifanyalo, kwa sababu lile nilipendalo silitendi, bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda.**

**16 Lakini kama nikilitenda lile nisilolipenda, nakiri ile sheria ya kuwa ni njema.**

**17 Basi sasa si mimi nafsi yangu ninayetenda hilo, baali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu.**

**18 Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu, halikai neno njema; kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo njema sipati.**

**19 Kwa maana lile njema nilipendalo, silitendi; bali lile mbaya nisilolipenda ndilo nilitendalo.**

**20 Basi kama lile nisilopenda ndilo nilitendalo, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu.**

**21 Basi nimeona sheria hii, ya kuwa kwangu nitakaye kutenda lililo njema, lipo lililo mbaya.**

**22 Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani, 23 lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kunifanya mateka ya ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu.**

**24 Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakeyeniokoa na mwili huu wa mauti?**

**25 Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Basi, kama ni hivyo, mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi.**

Unaweza kuona rahisi kukubaliana na mashindano anayopitia Paulo katika mistari hii. Anataka kufanya kilicho sawa, lakini anajikuta akienda kinyume. Ana hali ya uasi iliyo ndani ya moyo wake – siyo shetani. Ni moyo wake binafsi—njia zake za dhambi zinazomsukuma kila upande na kumnyima nguvu za kufanya maamuzi mema.

Wapaswa kufikia hitimisho lilelile alilofikia Paulo—huwezi kuwa mtiifu kwa nguvu zako mwenyewe. Unahitaji nguvu za Mungu kukusadia kuwatii viongozi wako. Mungu ameahidi kukupa nguvu wakati u dhaifu.

**2 Wakorintho 12:9**

**Naye akaniambia, neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu.**

**Wafilipi 4:19**

**Na Mungu wangu atawajazeni kila Mnachohitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.**

Unaweza kuamini kwamba Mungu atakupa nguvu zote unazohitaji kuwatii viongozi wako. Kila wakati yuko na nguvu za kutosha kwa ajili yako. Kuwajibu viongozi wako kwa njia ya kiungu kwaweza kuwa vigumu kwako, lakini Mungu kila mara yuko tayari kukusaidia. Kile unachopaswa kufanya tu ni kuomba msaada Wake.

## Kwa muhtasari

Umebeba ufunguo wa kufanya maisha yako kuwa mepesi au magumu zaidi—maisha yaliyojaa shida zaidi. Jinsi unavyowajibu viongozi wako yaweza kuleta amani maishani mwako, au kinyume.

Ufunguo halisi hapa ni kuhamisha mtazamo wako kwa yale unayoyataka na kuyatamani na kumuangalia Yesu. Mojawapo ya nidhamu bora ambayo waweza kukuza maishani mwako ni kujiuliza, “Yesu, ungependa ni mjibu kwa njia gani kiongozi wangu katika hali hii?” Jaribu kufikiria jinsi Yesu angejibu kama angekuwa katika nafasi yako akikabiliana na hali hiyo hiyo inayokukumba.

# Sura ya 4
# Unapaswa kufanya nini kiongozi wako akikwambia ufanye jambo ambalo sio sahihi?

Je, umewahi kuambiwa na mtu aliye katika mamlaka ufanye jambo lisilo sahihi? Katika akili yako waweza kufikiria kwa haraka kuhusu jambo kama "Je, itakuwaje ikiwa kiongozi wangu ataniambia niruke kutoka juu ya paa la jengo hili la gorofo 10?
Je, yapaswa nitii?"

Lakini hebu tuukabili ukweli uliopo. Ni mara ngapi umeambiwa na kiongozi wako ufanye jambo unaona sio sahihi? Mara nyingi unaambiwa ufanye mambo yaliyo *sahihi!* Yasiyo sahihi huenda ni 1 kwa 100 (au jambo moja kati ya 10,000) ambapo unaambiwa jambo lisilo sahihi na viongozi wako.

Soma kitabu cha mwongozo wa kufanya mazoezi nambari 3 na 5, inayozungumzia kuhusu Daniel sura ya 1 na 3. Sura hizi zinaelezea hali ambayo watu waliambiwa wafanye jambo lisilo sahihi na jinsi walivyowajibu viongozi wao. Watu hawa wanatupa mfano hai wa jinsi ya kuwajibu viongozi wetu kwa njia itakayomtukuza Mungu.

## A. Tathmini kwa makini kile umeambiwa kufanya

Badala tu ya kumjibu kiongozi wako kwa haraka, vuta pumzi, na funga kinywa chako—usiongee. Fikiria kwanza. Kisha muombe Mungu akusaidie kujibu kwa makini katika hali hii.

### 1. Tafuta kujua kama ulisikia vyema kile kiongozi wako alikuambia ufanye

Usidhanie kwamba ulisikia vyema. Ikiwa unafikiria kiongozi alikuambia ufanye jambo unaloamini sio sahihi, basi tulia. Usikimbilie uamuzi kwamba kiongozi wako amekosea na anajaribu kukuingiza katika dhambi.

Ongea na kiongozi wako ili kuhakikisha kwamba ulichokisikia ndicho alichokisema. Uliza swali lako kwa njia ambayo unahusisha kile unachofikiria kiongozi wako alikuambia ufanye. Usimlaumu au kumshtumu kiongozi wako.

Siku moja Doug alikuwa akikutana na kiongozi wake, wakijadiliana kuhusu mambo yalivyokuwa kazini mwake. Kiongozi alimwambia Doug kwenda kuwasilisha ujumbe maaalum kwa mtu aliyehusika katika hiyo shida. Lakini Doug alipofikiri kuhusu ujumbe ambao alipaswa kuwasilisha, ilkuwa ni wazi kwake kwamba ataulizwa kumdanganya huyo mtu. Kwa hivyo Doug akamgeukia kiongozi wake, ambaye alikuwa Mkristo na kumuuliza, “Je, unaniambia nimdanganye huyu mtu?”

Moja kwa moja kiongozi wa Doug alibadilisha ujumbe uliopaswa kuwasilishwa kwa huyo mtu katika hali hiyo. Hakuna hakika kwamba hali yako itasuluhishwa moja kwa moja kama ile ya Doug. Lakini wapaswa kuwa tayari kufanya jinsi Doug alivyofanya—muombe kiongozi wako aweke bayana.

Uliza swali lako kwa njia ambayo kiongozi wako ataona kwamba hautaki kuasi. Ikiwa hukumuelewa kiongozi wako, shida hiyo itasuluhishwa kwa haraka. Ikiwa ulisikia vyema mara ya kwanza, na unaamini unaambiwa ufanye jambo lisilo sahihi, basi unahitaji kufuata maagizo yanayofuata katika sura hii.

Usiogope kumuuliza kiongozi wako ikiwa ulielewa kile alichosema. Ikiwa utadhania ulielewa vyema, lakini hukuelewa, basi inaweza kuleta matokeo mabaya sana.

Jumapili moja asubuhi kanisani mke wa mchungaji alikuwa akicheza kinanda kabla ya kuanza ibada. Mwanachama wa kwaya aliingia na kumuuliza kuhusu moja ya nyimbo ambazo angeimba asubuhi hiyo. Kwa kuwa mchungaji ndiye alikuwa kiongozi wa kwaya hiyo, mke wa mchungaji alimuambia mwanachama huyo wa kikundi cha kwaya “Nenda kwa Hal” (jina la kwanza la mume wake). Mwanachama wa kwaya alifikiri amemuambia “Nenda kuzimu” na akaondoka huku amekasirika na mwenye uchungu. Alieneza uvumi kwamba mke wa mchungaji alimuambia aende kuzimu.

Ikiwa mwanachama wa kwaya angemuuliza mke wa mchungaji kama amemsikia vyema, hali hiyo yote ingesuluhishwa pale pale. Lakini kwasababu hakufanya hivyo, matokeo mabaya ya uvumi wake yalileta machungu makubwa na shida kwa huduma ya mchungaji na mke wake. Mwisho mbaya wa hadithi hii ni kwamba madhara yaliyosababishwa na kutoelewa huku yalikuwa makubwa kiasi ambacho mchungaji na mke wake waliondoka katika kanisa hili.

## 2. Chunguza kama ulichoambiwa ufanye ni dhambi hakika

Kwa makini tathmini amri au sheria uliyopewa. Kama ukitii, ni ipi kati ya sheria ya Mungu utaivunja? Au inaonekana sheria mbaya? Huenda ukafikiria haileti maana yoyote. Kwa mtazamo wako inaonekana kuwa sheria au uamuzi mbaya? Unafikiria kuna njia bora zaidi ya kufanya hiyo kazi? Unahisi kwamba kiongozi wako amefanya kosa kubwa kabisa?

Je, ni sheria ambayo inaonekana kuwa si sawa? Kwa mfano, hebu tuseme wewe na wengine mnaoishi na mna jukumu la kukamilisha kazi fulani nyumbani kila siku. Umepewa kazi mara tatu zaidi ya wengine. Hakuna muda wa ziada au mshahara wa ziada kwa wewe kufanya kazi saa zaidi. “Hili si sawa?” Unasema moyoni. Lakini je, ni dhambi? Je utakuwa ukivunja moja ya sheria za Mungu ikiwa utafanya kile ulichoambiwa ufanye?

Au pengine una hasira na kiongozi wako, hasa ikiwa alikuwa mkali alipokuwa akitaka ufanye hiyo kazi. Huenda ukahisi kwamba kiongozi wako anakosa kuwajibika. Lakini njia waliotumia kuwasliana nawe haikupi haki ya kutowatii.

Ikiwa kile ambacho kiongozi wako amekuambia ufanye si dhambi, basi una jukumu la kumtii kiongozi wako. Ikiwa sio dhambi, basi hali hiyo haingiliani na yale yatakayojadiliwa katika sura hii inayofuata. Una wajibu wa kumtii kiongozi wako hata kama haupendi amri iliyotolewa. Huenda utapenda kujadili hali hiyo na kiongozi wako, na uone kama unaweza kutoa maoni yako. Viwango vitatu vya utiifu vilivyojadiliwa katika somo hili kwa sasa vinaenda sawa na hali hii.

Kila wakati viongozi wako wanapokuambia ufanye jambo fulani, unapaswa kuiona kama fursa ya wewe kumtii Mungu, na ikiwezekana, viongozi wako duniani. Wakati kiongozi wako anapokuambia ufanye jambo ambalo ni dhambi, unapaswa kuchagua nani wa kumtii, Mungu, au kiongozi wako. Kwa hivyo ikiwa utachagua kutomtii kiongozi wako utakuwa unafanya hivyo kwasababu unataka kumtii Mungu.

### 3. Kama ni dhambi, amua ni dhambi ipi

Ikiwa una hakika kwamba kiongozi wako anakuammbia utende dhambi basi kuwa tayari kujibu swali hili linalofuata. Kwa kufanya kile kiongozi wako amekuambia ufanye ni ipi kati ya sheria za Mungu utakuwa umevunja?

Wakati mwingine kiongozi wako atakuambia ufanye jambo linalonekana wazi la kipumbavu. Utasema moyoni “Hilo haliwezi kuwa jambo sawa. Ni lazima iwe dhambi!” Lakini kuwa wazi. Tambua ni ipi kati ya sheria za Mungu utavunja ikiwa utamtii kiongozi wako.

Je, unaulizwa kusema uongo? Unaambiwa uibe?

Katika Agano la Kale, Yusufu alikuwa akifanya kazi kutoka nyumba ya Potifa. Kwa siku kadhaa mke wa Potifa alikua akimuuliza alale naye. Yusufu hakuhitaji kuomba ili kufahamu kwamba kile alichokuwa akiambiwa afanye ni dhambi. Alifahamu waziwazi kile ambacho mke wa Potifa alikuwa akitaka kutoka kwake, na alijua ikiwa angemtii, angekuwa akitenda dhambi kinyume na Mungu. Unaweza kusoma hadithi hii yote katika sura ya 39 ya kitabu cha Mwanzo.

## B. Gundua sababu kuu iliyomfanya kiongozi wako kukuambia ufanye hivyo

Hili ni ya muhimu sana! Ikiwa huelewi sababu kuu ya wao kukuuliza ufanye hivyo, basi hutaitikia kwa njia inayofaa. Pindi unapogundua sababu kuu ya kwa nini uliambiwa ufanye jambo lisilo sahihi, basi ni lazima uamue suala hilo liko katika kikundi kipi kati ya hivi vinne vilivyo hapa chini.

### 1. Je, sababu hii kuu ni kwa wema wako?

Je, sababu kuu sio dhambi? Angalia Danieli sura ya 1 kwa mfano wa kiongozi wa Danieli akitaka kilicho bora zaidi kwa vijana katika mafunzo. Kiongozi hakuwa anajaribu kuwaingiza Danieli na marafiki zake katika dhambi. Makusudi yake yalikuwa ni kuwapa kile alichofikiri kuwa ni lishe bora ili wawe na afya njema.

### 2. Je sababu kuu ni kukufanya utende dhambi?

Soma Mwanzo 39 na Danieli 3 kwa mifano miwili ya hii. Katika Mwanzo 39 Yusufu alikuwa mtumwa katika nyumba ya Potifa. Mke wa Potifa alimjaribu Yusufu alale naye. Ni wazi makusudi yake Mke wa Potifa yalikuwa kumfanya Yusufu atende kitendo cha kuvunja sheria za Mungu.

Katika Danieli 3 Shadraki, Meshaki, na Ebednego walikabiliwa na ibada ya sanamu. Waliamriwa kuinama na kuabudu sanamu iliyotengezwa kwa heshima ya mfalme. Watu hawa walielewa wazi kile walichoambiwa wafanye, na jinsi ilivyoenda kinyume kabisa na sheria ya Mungu. Viongozi wa nchi hiyo hawakujali kwa vyovyote vile sheria ya Mungu iliyosema kuhusu ibada ya miungu mingine.

### 3. Je, kiongozi wako anakujaribu ili kuona kile utakachofanya?

Angalia Mwanzo 22:1-19 na Waebrania 11:17-19. Mungu alimuambia Ibrahimu kwenda na kumuua na kumtolea mwanawe kama dhabihu. Ndiyo Mungu anatuambia tusiue. Mwanzo 22:1 inasema kwamba Mungu alikuwa akimjaribu Ibrahimu.

### 4. Kiongozi anafanya mzaha?

Wakati mwingine viongozi watakuambia ufanye jambo, lakini wanafanya mzaha tu na hakika hawajakusudia ufanye kile ambacho wamekuambia ufanye.

## C. Ikiwa sababu kuu ya kile ambacho kiongozi wako amekuambia ufanye ni kwa wema wako (na si dhambi), una jukumu la kutii

### 1. Tafuta njia nyingine ya kufanya jambo hilo ili usitende dhambi

Hakikisha kwamba njia yako (njia ya mbadala bunifu) inatimiza malengo ya kiongozi wako. Katika Danieli sura ya kwanza, Danieli alitafuta njia ya kujitunza kiafya. Njia yake haikuvunja sheria yoyote ya Mungu, ambapo amri ile ya kwanza ingevunja sheria za Mungu. Kuwa mbunifu! Jaribu kuifanya njia yako kuwa rahisi kwa kadri unavyoweza. Muombe na umuulize Mungu kukusaidia njia nyingine rahisi ya kufanya hivyo—njia ya mbadala bunifu.

### 2. Ongea na kiongozi wako

Hakikisha kwamba unaonyesha tabia za utiifu na nia ya kumtii kiongozi wako. Muambie unataka kumsadia atimize malengo yake.

Mpendekezee kiongozi wako njia utakayotumia kufanya hivyo. Mueleze ni kwa nini ungenpenda kuifanya kwa njia iliyo tofauti. Mueleze hali yote ilivyo. Usidai kiongozi wako akuruhusu kuifanya kwa njia yako. Usimlaumu wala kumshtumu kiongozi wako.

### 3. Mpe Mungu wakati wa kubadilisha mawazo ya kiongozi wako

Ikiwa Mungu anataka kubadilisha mawazo ya kiongozi wako, atamsukuma kiongozi wako. Kuwa tayari kusukumwa na kiongozi wako. Msukumo huu ni kwa manufaa yako, kukusadia kukuza tabia ambazo Mungu angependa uwe nazo.

## D. Ikiwa sababu kuu ya kiongozi wako kukuambia ufanye jambo hilo ni kukuingiza katika dhambi, basi una jukumu la kutomtii

Angalia Danieli 3 kama mfano mmoja wa hili. Ni muhumi kabisa kutambua kusudi wazi la kiongozi wako ni kukufanya utende dhambi. Unaposoma hadithi iliyo katika Danieli 3, unaona wanaume watatu wajasiri, lakini walio na heshima kwa mfalme.

Leo hii eneo moja ambalo Wakristo huambiwa watende dhambi ni katika maeneo yao ya kazi. Mkubwa wao anawaambia wabadilishe ripoti ili kufanya hali ionekane kwamba kila kitu ni sawa, na kufunika shida zilizopo hapo kazini. Ni wazi kwamba Mkristo anaambiwa adanganye.

Hali kama hii inakabiliwa na watu wanaouza bidhaa, wakati mkubwa wao anapowaambia wamdanganye mteja, ili kumshawishi anunue gari au bidhaa yoyote ile wanayouza.

### 1. Ongea na kiongozi wako

Onyesha heshima kwa kiongozi wako. Onyesha tabia ya utiifu kwa kiongozi wako.

Muulize kiongozi wako sababu kuu ya kukuuliza ufanye jambo hilo. Hakikisha uanelewa jibu. Pengine sababu yake kuu ni tofauti na jinsi ulivyofikiria. Pengine sababu yake kuu haikukusudia utende dhambi.

Muelezee kiongozi wako kwa nini unaamini hilo si sawa na kwa nini itabidi ukose kutii amri yake. Usimlaumu kiongozi wako wakati unapomulezea sababu ya kutotii kwako.

### 2. Mpe Mungu wakati wa kubadilisha mawazo ya kiongozi wako

Ikiwa Mungu anataka kubadilisha mawazo ya kiongozi wako, ataweka msukumo moyoni mwa kiongozi wako. Kuwa tayari kwa kiongozi wako kukusukuma hata zaidi. Msukumo huu ni kwa faida yako. Hii itakusaidia kukuza tabia ambayo anataka uwe nayo.

**Mithali 21:1**

**Moyo wa mfalme huwa katika mkono wa Bwana; kama mifereji ya maji huugeuza popote apendapo.**

Huu ni mstari mgumu katika Biblia. Ni mgumu kuuamini kwa sababu mara nyingi sisi hatukubaliani na baadhi ya maamuzi yanayotolewa na viongozi wetu. “Ikiwa Mungu anamuongoza kiongozi wangu, basi lazima Mungu awe amechanganyikiwa.”

Mstari huu haumaanishi kwamba Mungu hukubaliana na kila uamuzi unaotolewa na viongozi wako. Lakini ahadi yake iko wazi kwamba Mungu anawaangalia viongozi wako, na anaweza kuwaongoza kubadilisha maamuzi yao kama vile Mungu anavyoweza kubadilisha mkondo wa maji.

Sehemu ngumu kwako ni kumgoja Mungu, kumpa nafasi ya kile anachojua ni bora. Mara nyingi sisi hutaka mabadiliko ya mara moja kufanyika kwa wengine, lakini hilo huwa adimu kufanyika. Badala yake, tunahitaji kutafuta njia ya Mungu katika hali hii ngumu. Mungu ana hekima nyingi ya kukupa.

## 3. Kuwa tayari kuteseka kwa kufanya mambo yaliyo sahihi

Katika 1 Petro 2:20 tunapewa ushauri kuhusu kuteseka kwa kutenda yaliyo sahihi mbele za Mungu.

> **1 Petro 2:20**
>
> **Kwa maaana ni sifa gani kustahimili, mtendapo dhambi na kupigwa makofi? Lakini kustahimili mtendapo mema na kupata mateso, huu ndio wema hasa mbele ya Mungu.**

Maandiko haya yanazungumzia kuhusu hali mbili tofauti: kwanza, kuteseka kwa kutenda maovu. Pili, yanazungumzia kuhusu unapoteseka wakati unatenda mema kwa mtazamo wa Mungu. Ikiwa kiongozi wako atakataa kubadilisha mawazo yake, basi una jukumu la kutotii na kwa kimya uvumilie matokeo yake.

Kuchukua adhabu kwa ukimya silo jambo rahisi kufanya. Huenda ikamanisha kupoteza kazi. Siku amabyo Yesu alisulubiwa ni mfano mzuri wa matokeo ya kuteseka kwa ukimya kwa kufanya jambo lililo sahihi.

Mara nyingi kuteseka huku ni kwa manufaa yako. Kupoteza kazi yako kwawezaje kukufaidi? Unatakiwa ungalie hali hii kwa mtazamo wa kiungu. Kwanza, Mungu ni mpaji wako. Anaweza kubadilisha hali hii ngumu kwa wema wako.

Mungu huenda akakupa kazi iliyo bora hata zaidi. Lakini hata kama hatafanya hivyo, na upate kazi iliyo na mshahara mdogo, unaweza kuwa na ujasiri kwamba Mungu yuko nawe. Kuwa na dhamiri safi ni jambo njema kuliko kuishi katika dhambi na kuwa na kazi inayolipa mshahara mkubwa.

Mungu anataka kutumia hali hizi ili kujenga ndani yako sifa unazohitaji kama Mkristo aliyefanikiwa. Mara nyingi sisi huteseka, kwa sababu ya mojawapo ya mambo haya:

1. Tabia zetu mbaya
2. Ukosefu wetu wa kuwa wabunifu
3. Kutotii kwetu

Tunapojitahidi kumtii Mungu, tunaweza kuwa na imani kwamba atatusaidia kukua. Yusufu katika sura ya 39 ya kitabu cha Mwanzo alimtii Mungu, lakini mwisho alimalizia gerezani kwa ajili ya matendo yake. Hata katika gereza, alizidi kumtumikia Mungu na mwishowe Mungu alimtumia kwa njia kuu sana kama msaidizi wa Farao, nchini Misri.

## 4. Toka katika hali ya kunyanyaswa

Wakati mwingine watu hukumbwa na hali ya kunyanyaswa. Binti mmoja mwenye umri wa miaka 21 alikuwa akiishi na baba yake aliyekuwa akimnyanyasa kimapenzi katika maisha yake ya ujana. Hata akiwa na umri wa miaka 21, baba yake bado alikuwa akimnyanyasa kimapenzi. Wakati huo huo alipokuwa akimdhulumu kimapenzi, alikuwa bado akitumika kanisani mwao, akiwa anaheshimiwa sana kanisani.

Tamaduni zao za nyumbani na kanisani zilithamini sana jambo la kuwaheshimu wazazi wako. Hata japo alifahamu kile alichokuwa akifanya baba yake hakikuwa sahihi, hakuwa na ujasiri wa kufichua dhambi yake. Ijapokuwa alitafuta msaada wa mshauri wa Kikristo, hakuwa tayari kuondoka kwa jamii yao, na kutomheshimu baba yake.

Mtu anapaswa kufanya nini akijikuta katika hali hii ya kunyanyaswa? Hatua zilizo katika sura hii hazifanyi kazi katika aina hii ya dhambi. Huhitaji kukaa katika hali kama hiyo, na "Umpe Mungu nafasi ya kubadilisha mawazo ya mtu huyo."

Biblia iko wazi—dhambi yapaswa kufichuliwa. Kamwe si mapezi ya Mungu kumruhusu mtu kukunyanyasa kimapenzi au kukupiga. Hatua ya kwanza ni kutoka katika hali hiyo ya kunyanyaswa—mara moja. Kisha unatakiwa uchukue hatua za kujilinda dhidi ya kunyanyaswa zaidi. Ni lazima uwe karibu na watu watakao kuweka salama.

## Mukhtasari

Sura hii nzima imejadili suala gumu sana. Ni matarajio yangu kwamba hutakumbana na aina hii ya shida kila mara. Lakini shida zikikujia, unahitaji kuomba na kutafuta msaada wa Mungu utakaokuwezesha kuitikia kwa njia itakayomtukuza.

Yusufu na Danieli wote wanatoa mfano wazi wa jinsi unavyoweza kutowatii viongozi wako kwa njia inayomheshimu Mungu. Watu hawa wote walikuwa na uhusiano wa kina sana na Mungu na shauku ya kuwa watiifu. Shauku yao ya kumtii Mungu ndiyo iliyowasukuma kutowatii viongozi wao. Hawakuwa wanakosa kutii kwa moyo wa uasi. Wakati huo huo walipokuwa wakikosa kuwatii viongozi wao, walikuwa wakifanya kila wanaloweza kumtii Mungu.

Hata wakati unakumbana na hali ngumu, ikiwa umejitolea kwa vyovyote vile kumtii Mungu, atakupa nguvu na hekima ya kufanya maamuzi sahihi.

# Sura ya 5
# Matokeo ya kutii na kutotii viongozi wako

Huhitaji kuangalia mbali kuona matokeo ya kutii au kutotii viongozi wako. Mara nyingi sisi hukosa kufikiria kuhusu matokeo ya kutii au kutotii wakati tunapokumbana na jaribu la kutomtii kiongozi. Biblia inatoa mifano kadhaa ya kile kinachofanyika wakati mtu anapowatii au kutowatii wale walio katika mamlaka.

Unapotazama matokeo ya kuwatii na kutowatii viongozi wako, hili laweza kuwa nguvu ya kukutia motisha kuwatii viongozi wako. Ni rahisi sana kuona hali ilivyo kwa sasa na kusema, “Huu ni ujinga. Sitafanya hilo. Najua kilicho chema kwangu.”

Lakini ikiwa utatulia na uangalie kwa makini matokeo ya kutii na kutotii viongozi wako, utaanza kuona matokeo ya siku zijazo ya maamuzi yako. Usiruhusu hisia zako za wakati huu kukuibia faida za utiifu wa siku zijazo na matokeo haribifu ya kutotii.

## A. Matokeo ya kuwatii viongozi wako

Unapochagua kuwatii viongozi wako, mara utaona faida ya maamuzi haya ya hekima. Huenda kwa kupitia uzoefu wako umefahamu kwamba kuwatii viongozi wako hakuondoi shida zako zote. Hakika, wakati mwingine kuwatii viongozi wako ni kazi ngumu, na huleta shida nyingi zaidi. Biblia haiahidi kwamba maisha yatakuwa yenye tabasamu na furaha kwa kuwa tu umewatii viongozi wako.

Utiifu waweza kuwa mgumu hapo mwanzo, lakini faida za baadaye huoenekana kadiri muda unavyoendelea kusonga.

### 1. Utiifu huathiri kivipi uhusiano wangu na wengine?

Utiifu huathiri uhusiano wako na wetu wengi siyo tu huyo kiongozi mmoja aliyekuambia la kufanya. Fikiria kuhusu hali ya hivi karibuni ambapo ulimtii kiongozi wako. Kisha uliza swali hili kuhusu hali yako. “Ni kwa njia ipi kumtii kwangu kiongozi huyu kuliathiri uhusiano wangu na watu hawa?”

1. Mungu
2. Wazazi wangu na familia

3. Watoto wangu (waliopo na wajao)
4. Rafiki zangu
5. Ninaofanya kazi nao
6. Watu wengine walio karibu nami

Somo moja ambalo waweza kujifunza kutoka kwa maisha yako ni kwamba, utiifu ndiyo njia ya kuwa na mahusiano mema. Utiifu hujenga madaraja kupitia kwa watu, lakini kutotii huvunja mahusiano na watu wengine. Utiifu ndiyo njia ya kukomaa.

Wakati Yesu alipokuwa kijana anayekua nyumbani mwa wazazi wake, Biblia inasema alikua katika hekima na kupata kibali cha Mungu na wanadamu kwa kuwa aliishi maisha ya utiifu.

**Luka 2:51-52**

**Akashuka pamoja nao hadi Nazarethi, naye alikuwa akiwatii …. (Yusufu na Maria)… 52 Naye akaendelea kukua katika hekima na kimo; akimpendeza Mungu na wanadamu.**

## 2. Mungu huona vipi utiifu?

Bibilia inasema wazi kwamba shida nyingi zaweza kuepukika ikiwa tutawatii viongozi wetu. Zoezi la saba katika kitabu chako cha Somo kinakuuliza kuandika orodha ya matokeo ya wewe kuwatii viongozi wako.

Hapa kuna maandiko machache, ambayo yanaonyesha matokeo ya kutii.

1. Mwanzo 24
2. 1 Wafalme 17:8-23
3. Mithali 2:01-02
4. Mithali 6:20-24
5. Mithali 13:13
6. Mithali 28:7
7. Warumi 13:1-6
8. Waefeso 6:1-3
9. Waefeso 6:5-8
10. Waebrania 5:8-9, Waebrania 13:17
11. 1 Petro 2:13-17

Kuna maandiko mengi katika Biblia yanayofunza somo hili—Mungu analipa kipaumbele suala la sisi kujifunza kuwatii viongozi wetu. Biblia pia iko wazi kwa kusema kwamba Mungu ameahidi kutubariki ikiwa tutawatii viongozi wetu.

## 3. Ni kwa jinsi gani utiifu unabadilisha maisha yangu?

Unapokuza tabia za utiifu tulizozungumzia katka sura ya 1, hii itakurahizishia kuwatii viongozi wako. Matendo ya kutii yatabadilisha maisha yako. Utiifu hukusaidia kukuza tabia njema maishani mwako. Hebu tuangalie kwa makini mambo mawili kati ya haya—nidhamu ya kibinafsi na imani.

### a. Kukuza nidhamu ya kibinafsi

Katika sura ya 2 tulizungumzia kuhusu kukuza viwango vitatu vya utiifu. Unapofanya kazi ili kufanya viwango hivi vitatu sehemu ya maisha yako ya kila siku, unaweza kukua katika eneo la nidhamu ya kibinafsi. Unaamua kufanya jambo lililo sahihi kivyako, sio tu kuepuka matokeo yaliyo machungu, lakini kwa sababu ni jambo sahihi kufanya.
Unajua kwamba utiifu humependeza Mungu.

**Viwango vitatu vya utiifu**

1. Tii kwa kuwa uliambiwa ufanye hivyo.
2. Tii na ugundue sababu kuu ambayo ilimfanya kiongozi wako akuambie ufanye.
3. Tii kwa hiari yako—kwa sababu ni jambo sahihi kufanya.

Nidhamu ni kuishi katika ile mipaka ambayo wewe na viongozi wako mmeweka. Kadiri unavyokuza nidhamu ya kibinafsi, ndivyo itakavyokuwa rahisi kwako kupinga majaribu ya kutenda dhambi.

### b. Kukua kwa kuamini

Utiifu hutusadia kukuza sifa ya kuamini. Unapojifunza kumuamini Mungu unaweza kuamini kwamba atatumia utiifu wako kwa viongozi wako kukusaidia uwe yule mtu ambaye amekusudia uwe.

Kuamini hukusaidia kukua hadi kiwango cha kusema, “Naweza waamini viongozi wangu kwa kuwa namuamini Mungu.” Hii sio imani pofu. Lakini ni imani iliyopimwa. Bado unatakiwa kuja kwa Mungu akuelekeze jinsi ya kuwajibu viongozi wako.
Wakati wanapofanya makosa, unawezaje kuhusiana vyema nao?

Hata wakati unapatwa na shida kwa kuwa viongozi wako hufanya makosa, au wanapungukiwa kwa njia moja au nyingine, unaweza kuwa na ujasiri kuwa Mungu hakufanya makosa yoyote kwa kukuruhusu upitie hali hiyo. Unapowatii viongozi wako, na kuendelea kukua, unaweza kujifunza kuwaamini viongozi wako jinsi Mungu anavyotaka uwaamini.

# B. Matokeo ya kutowatii viongozi wako

Ni rahisi sana kuhalalisha kutotii, hasa ikiwa ni wewe unafanya! Pengine ulidhani hii ni sheria ya kiujinga, au ulishawishika kwamba kiongozi hakuwa anafanya vyema. Huenda ukafikiria kuhusu sababu nyingine nyingi nzuri ambazo watu hutoa kwa kutotii. Hata hivyo, sababu hizi zote hazibadilishi ukweli kwamba ilikuwa tabia ya kutotii. Tayari tumekwisha jadili hali zile adimu ambapo viongozi wetu hutuambia tufanye jambo litakalovunja mojawapo wa sheria za Mungu.

Kuna matokeo wazi ya kuzivunja sheria na kanuni zilizowekwa na viongozi wetu. Wakati mwingine matokeo huoenekana mara moja, hasa wakati askari anapowaona watu ambao hawakusimama wakati taa nyekundu ilipowaka.

Wakati matokeo hayaji mara moja, watu wengine hujidanganya wakifikiria kwamba wataepuka kwa kutotii kwao. Watu wengine hawaoni matokeo ya kutotii kwao.

Mungu ameweka wazi kwamba yeye huwa hapuuzi tabia ya kutotii. Ikiwa adhabu ya dhambi haiji katika maisha haya, mtu huyu atapata hukumu baada ya kifo.

## 1. Matokeo ya kutowatii viongozi wako?

Kuna aina nne ya matokeo tofauti ambayo mara nyingi yanahusiana na matendo ya kutotii. Tunapaswa kuangalia kwa makini kwa kila moja ya haya matokeo ili tupate kuelewa jinsi kila moja inavyohusiana na kutotii.

### a. Matokeo ya kiasili

Mzazi anaelezea mtoto wake, “Usiguse jiko. Ni moto sana.” Ikiwa mtoto atakosa kutii na kugusa lile jiko, **matokeo asili** ya kitendo hicho cha kutotii ni kwamba mtoto huyo huenda akachoma vidole vyake.

Matokeo ya kawaida ni hayo tu – kawaida (moja kwa moja) matokeo ya kitendo fulani. Matokeo haya hayafanani na nidhamu au adhabu. Unapokosa kuwatii viongozi wako, mara nyingi huwa na matokeo. Huenda usishikwe kila wakati unapokosa kuwatii viongozi wako, lakini kila mara kutakuwa na athari zitakazobaki kwa kutotii kwako.

Matokeo mojawapo mabaya sana ya kutotii ni kwamba utaanza kukuza tabia ambazo zitafanya iwe rahisi kwako kutotii. Tabia hizi za kutotii zinafanya iwe vigumu sana kwako kuwatii viongzozi wako katika hali za siku zijazo. Angalia Wagalatia 6:7-10.

### b. Nidhamu

Wakati unakosa kuwatii viongozi wako, mara nyingi watakunidhamisha. **Nidhamu** inabeba dhana ya kurekebisha shida. Lengo la nidhamu nikukusaidia kuishi maisha sawa – kuamua kutii wakati unakumbana na hali sawa na hiyo. Waebrenia 12:7-11 inaelezea sababu ya viongozi wako kukunidhamisha.

**Waebrania 12:7-11**

**7 Ni kwa ajili ya kurudiwa mwastahimili; Mungu awatendea kama wana; maana ni mwana yupi asiyerudiwa na babaye?**

**8 Basi kama mkiwa hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, ndipo mmekuwa wana wa haramu ninyi, wala si wana wa halali.**

**9 Na pamoja na hayo tulikuwa na baba zetu wa mwili walioturudi, nasi tukawastahi; basi si afadhali sana kujitia chini ya baba wa roho zetu na kuishi?**

**10 Maana ni hakika, hao kwa siku chache waliturudi kama walivyoona vyema wenyewe; bali yeye kwa faida yetu, ili tushiriki utakatifu wake.**

**11 Kila adhabu wakati wake haionekani kitu cha furaha, bali cha huzuni; lakini baadaye huwaletea wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani.**

Tafsiri ya Biblia inatumia neno "adhabu" badala ya nidhamu. Katika hali hii, mtafsiri hatoi tofauti finyu kati adhabu na nidhamu ambayo tunayoizungumzia katika somo hii. Katika hali nyingi, neno adhabu linatumika katika mtazamo mpana kuhusisha aina yoyote ya nidhamu na kurekebisha.

Nidhamu inabeba ndani yake kipengele cha tumaini. Nidhamu inataolewa kwa tumaini kwamba italeta mabadiliko katika maisha ya mtu asiye mtiifu. Haijalishi ni aina gani ya nidhamu iliyotumiwa lazima iwe na matokeo wazi yatakayomuelekeza mtu katika kuelewa vyema njia bora ya kuishi.

Kadiri unapojifunza masomo ya nidhamu kwa haraka, ndivyo utakavyofanya maisha yako kuwa rahisi. Kutotii kutakupeleka katika njia ya maangamizi. Nidhamu imekusudiwa kukuweka katika njia inayofaa – njia inayoelekea katika maisha ya kweli.

### c. Adhabu

Adhabu, kama vile tunavyoielezea hapa, inabeba dhana ya hali fulani ya uchungu kwa yule ambaye ametenda kitendo cha kutotii. Adhabu inabeba dhana kwamba, unapakosa kuwatii viongozi wako, unapaswa kuteseka kwa matendo yako.

Adhabu mara nyingi haihusishi lengo la kukusaidia kurekebisha shida iliyopo. Inazingatia kulipia kosa uliofanya. Moja ya malengo ya adhabu ni kukufanya usikie uchungu sana kiasi cha kwamba utaacha tabia yako ya kutotii.

Adhabu mara nyingi haihusishi hali ya kumfunza mtu kuwa mtiifu. Hilo ndilo lengo la kimsingi la nidhamu. Adhabu inajengwa katika kanuni ya maisha kwamba "uchungu humtia mtu motisha ya kubadilika."

Katika jamii yetu, unaweza kuambiwa kulipa faini ikiwa utavunja sheria fulani, kwa mfano ukivunja sheria ya trafiki. Matendo mengine ya kutotii hubeba adhabu nzito zaidi, ikiwemo kufungwa jela.

### d. Kulipiza kisasi

Kulipiza kisasi hulenga katika kumlipa yule mtu aliyefanya kosa. Ikiwa Jim atampiga binti yako, basi utampiga Jim, au umtafute mojawapo ya marafiki zako wampige kwa niaba yako. Kulipiza kisasi ni kuchukua jukumu la kibinafsi la kumuadhibu mtu aliyekosa.

Kulipiza kisasi hupuuza mahusiano na mamlaka na majukumu walio nayo viongozi ya kuona kwamba nidhamu inayofaa imechukuliwa dhidi ya mtu aliyekosa kutii.
Warumi 12:17-21 inaelezea kile anachopaswa kufanya Mkristo kuhusu kulipiza kisasi. Mungu anasema.

**Warumi 12:17-21**

**17 Msimlipe mtu uovu kwa uovu. Angalieni yaliyo mema machoni pa watu wote.**

**18 Kama yamkini, kwa upande wenu, mkae katika amani na watu wote.**

**19 Wapenzi, msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu; maana imeandikwa, kisasi ni juu yangu mimi, mimi nitalipa, anena Bwana.**

**20 Lakini, Adui yako akiwa na njaa, mlishe; akiwa na kiu, mnyeshwe; maana ufanyapo hivyo, utampalia makaa ya moto kichwani pake.**

**21 Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema.**

Unapolipa kisasi kwa waliokukosea, unaingilia katika kwa kile ambacho Mungu angefanya katika hali hii. Huenda ikawa ni vigumu sana, lakini unahitaji kujifunza kuweka hali hizi za uchungu kwa Mungu na kumuambia, “Bwana, naachilia haki zangu za kulipiza kisasi kwa mtu huyu.”

## 2. Ni kwa jinsi gani kutokutii kunaathiri mahusiano yangu na wengine?

Kutotii huathiri mahusiano yako na watu wengi, siyo tu huyo kiongozi mmoja aliyekuambia cha kufanya. Mara nyingi huwa hatufikirii jinsi kutotii kwetu kutathiri wengine. Fikiria kuhusu tukio la hivi karibuni ambapo ulikosa kumtii kiongozi wako. Kisha uliza swali hili kuhusu hali hiyo. “Ni kwa njia gani tabia yangu ya kutotii iliathiri uhusiano wangu na watu hawa?”

1. Mungu
2. Wazazi na familia yangu
3. Watoto wangu (sasa na wa baadaye)
4. Marafiki zangu
5. Wale tunaofanya kazi nao
6. Watu wengine wanaoishi karibu nawe

Wakati unapoamini ni SAWA kutotii viongozi wako, unaweka katika matendo mfululizo wa matukio. Kutotii huibua migogoro. Wakati kutotii kunapoleta migogoro katika mahusiano, mara nyingi hufanya mahusiano hayo yakavunjika, hasa unapokataa kukubali kutotii kwako kulikuwa si sawa.

## 3. Mungu ana mtazamo gani kuhusu uasi?

Biblia inatoa mifano kadhaa ya nini kilichofanyika wakati watu walikosa kutii wale waliokuwa kwenye mamlaka. Zoezi la 8 katika Kitabu chako cha Somo linakuuliza kutoa orodha ya matokeo ya kutotii viongozi wako. Hapa kuna maandiko machache yanayozungumzia kuhusu kutotii.

1. Mwanzo 39
2. 1 Samweli 13 na 14
3. Mithali 13:13
4. Mithali 5:12-14
5. Mithali 15:9-10
6. Matendo 5:17-41
7. Warumi 13:1-6
8. 2 Wakorintho 10:6
9. 1 Petro 2:13-17

Ni hadithi zipi nyingine au mistari ipi katika Biblia ambayo umeipata inayoelezea kuhusu kutotii? Andika mistari hiyo kando ya hii iliyotajwa hapo juu.

Mungu anaweka wazi kwamba tunapokosa kutii viongozi wetu, hakika tunakosa kumtii. Tuliona katika hali zisizo za kawaida kwa jambo hili katika sura ya 4.

Kutotii huzaa upofu wa kiroho. Matendo yetu ya kutotii mara nyingi yamefichwa katika dhana zinazosema, kwa mfano, “Najua kilicho kizuri kwangu. Hakuna atakaye nilazimisha kufanya jambo la kipuuzi kama hili!”

Huwa umegeuza mgongo wako kinyume na Mungu wakati unakosa kuwatii viongozi wako. Unaelekea katika barabara ya uharibifu na giza. Ikiwa hutaacha, kutotii kutakuelekeza katika maangamizi. Unahitaji kujiangalia kwa kweli, na ujiulize, “Je, ninaacha roho ya utundu maishani mwangu kunizuia kuona kile kizuri ambacho Mungu yuko nacho kwangu?”

## 4. Hitaji la nidhamu na adhabu leo hii

Kwa kusoma tu kitabu hiki kuhusu utiifu hakuwezi kubadilisha maisha yako moja kwa moja. Tumeangalia jinsi unaweza kuwatii viongozi wako. Tumejadili faida za utiifu na matokeo mabaya yanayotokana na kutotii viongozi wako.

Lakini suala hili la utiifu sio tu nadharia. Sisi sote hukumbana na hali hii – karibu kila siku tunakumbana na hali ya kutoa uamuzi – nitatii au nitakosa kutii? Hili silo somo la kususbiri miezi sita au kwa mwaka mmoja kabla hujatekeleza. Huenda fursa ya kutekeleza mambo haya maishani mwako ikatokea saa chache zijazo, kama si hivi karibuni.

Wengi wetu wakati mwingine hushindana na utiifu. Matendo yako ya kutotii yanafunua hitaji lako la nidhamu. Mungu ameweka viongozi maishani mwako, na mojawapo ya jukumu lao ni kukunidhamisha wakati unapokosa kutii. Viongozi wengine wanaweza kukataa jukumu lao la kiungu na kukosa kukunidhamisha.Wengine huenda wakapita mipaka na kukuadhibu kwa njia amabayo haimpendezi Mungu.

Kwa hivyo unanidhamishwa au kuadhibiwa, Mungu anakupa fursa ya kubadilika – kukua. Uamuzi ni wako. Utajibu vipi?

> **Waebrania 12:11**
>
> **Kila adhabu wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha, bali cha huzuni, lakini baadaye huwaletea wale waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani.**

Ni njia gani za nidhamu zitakuwa za manufaa kwako? Hili ni swali gumu kwa wengi wa viongozi kujibu. Ni kwa njia gani wanaweza kukunidhamisha kiasi cha kukusaidia kupata mabadiliko ambayo Mungu anataka uwe nayo maishani?

Kama tayari uko katika nafasi ya uongozi na unapaswa kuwadhamisha wengine – watoto wako, wafanyi kazi pamoja nawe kazini mwako, au katika mazingira mengine – basi una jukumu la ziada. Wawezaje kuwanidhamisha watu katika njia itakayomtukuza Mungu?

Jambo moja liko wazi – nidhamu huenda ikawa sehemu ya maisha yako kwa miaka mingi ijayo, kwa sababu sote tutakutana na fursa nyingi za kutotii. Ni masikitiko kusema, wengi wetu watapungukiwa na kanuni ya Mungu ya utiifu, na tutahitaji kunidhamishwa.

## Mwisho

Kuwatii viongozi wako huenda ni mojawapo wa masomo yaliyo magumu kujifunza maishani. Hata hivyo, Kadiri unapofanya utiifu kuwa sehemu ya maisha yako ya kila siku, ndipo kwa haraka utapokea manufa yanayoambatana na utiifu.

Utiifu ni sehemu moja ya muhimu katika kukua – kuwa mtu aliyekomaa kama vile Mungu alivyokusudia uwe. Kumekuwa na vita maishani mwako, na huenda vita hivyo bado vinaendelea hadi leo. Kuamua kutii au kutotii huenda ni vita vya kila siku kwako.

Unapokusudia kuweka katika matendo viwango vitatu vya utiifu maishani mwako, unaweza kuwa na uhakika kwamba vitakuongoza katika njia kuu ya amani. Hii pia ni njia ya kukuza mahusiano mema na wengine. Usikubali chochote chini ya kile kilicho bora zaidi ambacho Mungu amekupangia.